





Issue no: 01 | Vol no: 06 | December 2025: 94-103

Lugha, Mawasiliano na Mizozo: Mikakati ya Mawasiliano katika Kesi za Mizozo kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu

Ogonda Samuel Sinzore ⁽¹⁾  ID
Eddah Martha Njeri ⁽²⁾  ID

(1) Kibabii University, Kenya; (2) Maseno University, Kenya.
Main author's email: sasio.ogonda@gmail.com

Article History

Received: 2025.10.13

Accepted: 2025.11.17

Published: 2025.12.14

Cite this article in APA

Ogonda, S. S., & Njeri, E. M. (2025). Lugha, mawasiliano na mizozo: Mikakati ya mawasiliano katika kesi za mizozo kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu. *Editon consortium journal of kiswahili*, 6(1), 94-103. <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.693>

Ikisiri

Makala hii inalenga kuchunguza mikakati ya mawasiliano inayotumika katika kesi za migogoro ya umiliki wa ardhi katika Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ujihusishaji iliyoasisiwa na Giles (1973) na kuendelezwa na Giles et al. (1991). Nadharia hii inaeleza kuwa washiriki katika mawasiliano hubadilisha matumizi yao ya lugha kulingana na muktadha, utambulisho na malengo ya mazungumzo. Data ilikusanywa nyanjani kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu. Kundi lengwa lilikuwa mawasiliano ya kesi sita ambazo zilikuwa zimeratibiwa kusikizwa katika mahakama hiyo mwezi wa Oktoba 2019. Usampulishaji wa dhamira ulitumiwa kuteua Mahakama ya Juu pamoja na kesi nne ambazo ziliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Mbinu ya uchunguzi usio wa kushiriki ulitumika kukusanya data. Baada ya data kukusanywa, ilipangwa na kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mawakili, hakimu, walalamishi na washtakiwa hutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano ambayo inaweza kuibua migogoro ya kimawasiliano au kuimarisha maelewano kati ya washiriki. Mikakati hii huwa na athari kubwa katika ufanisi wa mchakato wa maamuzi ya kesi. Makala hii inaonyesha kuwa lugha hutumiwa kama chombo muhimu cha utatuzi wa migogoro, lakini matumizi yake yanategemea sana mikakati ya mawasiliano yanayochaguliwa na washiriki. Makala hii inapendekeza kuwa, mahakama ihimze kutumiwa kwa mikakati ya mawasiliano ambayo itachochea athari chanya katika mawasiliano licha ya tofauti za kimamlaka baina ya wazungumzaji. Aidha, watafiti wa baadaye wachunguze mikakati ya mawasiliano inayotumika kupitia njia ya kidijitali kwa kuwa hivi karibuni, vikao vya mahakama vinaendeshwa kupitia mitandao.

Key words: Lugha, mahakama, mikakati ya mawasiliano, mizozo, ujihusishaji.



This article is distributed under the license of a [Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/). It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

UTANGULIZI

Makala hii inashughulikia mikakati ya mawasiliano katika kesi za mizozo ya umiliki wa ardhi kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu. Ingawa mfumo wa mahakama unalenga kutoa haki kupitia mawasiliano, uhalisia unabainisha kuwa mikakati ya mawasiliano inayoendeshwa na washiriki mahakamani hujengwa kupitia lugha kama chombo cha utekelezaji wa mikakati hiyo. Selinker (1972) anaiona mikakati ya mawasiliano kuwa mbinu zinazotumika kurahisisha mawasiliano. Hata hivyo, kuna changamoto zinazojitokeza katika jinsi mikakati hii inavyotumiwa na washiriki wa mahakama, hasa hakimu, mawakili, walalamishi, washtakiwa na mashahidi. Ingawa Seedhouse (2004) anaona lugha kama njia ya kuwawezesha washiriki kujenga maelewano katika mawasiliano, kuna uwezekano pia wa lugha kuwa chanzo cha migogoro ya kimawasiliano kupitia mikakati ya mawasiliano. Katika muktadha wa mahakama, hali hii huathiriwa na mambo kadhaa, ikiwemo madaraka ya washiriki, malengo yao na muktadha wa kijamii (Giles et al., 1991).

Kuna tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu matumizi ya mikakati ya mawasiliano katika mazingira ya mahakama (Anyonje, 2004; Kiguru, 2014; Magiri, 2019; Matu et al., 2012; Njeri et al., 2018; Obange & Wagah, 2019; Odera et al., 2019; Opeibi, 2012). Nyingi ya tafiti hizi zimejikita katika kuangazia aina ya mikakati ya mawasiliano kwa ujumla bila kuchunguza kwa kina jinsi lugha inavyoathiri utekelezaji wake katika mawasiliano, hasa kwenye mahakama. Mathalani, Matu et al. (2012) walichunguza nafasi ya tafsiri katika mawasiliano mahakamani na kubainisha umuhimu wake katika kuwawezesha wahusika kuelewana, pamoja na changamoto za uhamishaji wa maana zinazotokana na tafsiri. Widodo (2025) alichunguza sifa za mawasiliano katika kesi za jinai katika mahakama za Indonesia. Kupitia utafiti wake, Widodo anabainisha kuwa lugha hutumika kuendeleza ufafanuzi katika mawasiliano kupitia mbinu ya urudiaji na urekebishaji wa kauli. Utafiti wake unaonyesha matumizi ya mkakati wa mazungumzo katika mawasiliano mahakamani. Hii inaashiria kuwa mikakati ya mawasiliano mahakamani huathiriwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya lugha katika kujenga maelewano baina ya washiriki.

Aidha, tafiti nyingine zilijikita katika kuchunguza suala la mgawanyiko wa nguvu na madaraka baina ya wazungumzaji katika mawasiliano ya mahakama. Kiguru (2014) anabainisha hili kupitia mkakati wa maswali, ambapo anasema hudhihirisha tofauti hii hasa kati ya mawakili na washtakiwa au mashahidi ambao huwa hawajawakilishwa na mawakili. Richard na Nwizug (2017) wanabainisha kuwa mkakati wa mazungumzo ya kupokezana zamu unapotumika, kuna uwezekano wa hakimu kubatilisha au kukubali pingamizi za mawakili na hivyo kuathiri maamuzi ya kesi. Isitoshe, tofauti katika viwango vya umahiri wa lugha miongoni mwa washiriki, pamoja na sheria za mawasiliano katika muktadha wa mahakama zinazowapendelea maofisa wa korti (Luchjenbroers, 1993; Njeri et al., 2018), huathiri jinsi mikakati ya mawasiliano inavyotumika na washiriki mahakamani.

Hivi karibuni, kumeshuhudiwa ongezeko kubwa la mizozo ya ardhi ambayo mara nyingi huwasilishwa mahakamani ili isikizwe na kutatuliwa. Jiji la Kisumu limekumbwa na changamoto hii kutokana na ukuaji wa jiji lake (Obange & Wagah, 2019). Ongezeko hili la migogoro ya umiliki wa ardhi katika jiji hili linaashiria hitaji la kuchunguzwa kwa mikakati ya mawasiliano inayotumika katika mahakama ili kuboresha maelewano baina ya washiriki na mchakato wenyewe wa utatuzi wa mizozo.

Isitoshe, ufanisi wa mawasiliano katika kesi za ardhi zinazowasilishwa mahakamani hutegemea jinsi lugha inavyotumika kuimarisha mikakati ya mawasiliano baina ya washiriki ili kuwezesha kutatuliwa kwa migogoro hiyo. Linapofanyika hivyo, kutakuwa na uwezekano mkubwa wa migogoro ya ardhi iliyowasilishwa mahakamani kufikia kikomo badala ya kutokamilika haraka. Ni kutokana na mapengo haya ndipo kazi hii ilichunguza mikakati ya mawasiliano katika kesi za mizozo ya umiliki wa ardhi kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu.

MAPITIO YA MAANDISHI

Tafiti mbalimbali zilizofanywa zimeonyesha umuhimu mkubwa wa mawasiliano katika uendeshaji wa kesi mahakamani. Lugha inayotumika kuwasiliana hufungamana sana na mikakati ya mawasiliano na huamua ufanisi wa mikakati hiyo katika mchakato mzima wa utatuzi wa mizozo. Mathalani, Hale (2010)

anabainisha namna matumizi ya mkakati wa tafsiri yanavyoathiri uelewa wa ushahidi kutokana na uteuzi wa maneno pamoja na mtindo wa usemi wa mkalimani katika mahakama. Imebainika kuwa matumizi ya maswali ya moja kwa moja mahakamani ni mkakati ambao hutumiwa na mawakili pamoja na hakimu kudhibiti majibu yanayotolewa na mashahidi na pia kudhibiti mwelekeo wa mawasiliano (Gibbons, 2003; Kiguru, 2019). Wataalamu hawa wanabainisha kuwa hili hudhahirika kupitia matumizi ya istilahi za kisheria ambazo huenda zisieleweke kikamilifu na mashahidi, pamoja na uchaguzi wa maneno mahususi yanayotumika kufunga aina ya majibu yanayotolewa. Magiri (2019) alichunguza matumizi ya upatanisho kama mkakati wa mawasiliano na kubainisha kuwa ufanisi wa mbinu hii hutegemea matumizi ya lugha ya upole pamoja na kushirikishwa kwa mazungumzo katika mawasiliano. Kwa pamoja, tafiti hizi zimejikita zaidi katika kuchambua lugha na mikakati ya mawasiliano bila kubainisha kwa kina jinsi zinavyoathiri mawasiliano yenyewe.

Vilevile, mawasiliano mahakamani yamebainisha kudhibitiwa na tofauti za kimamlaka baina ya washiriki. Kwa mfano, Odera et al. (2019) wanabainisha kuwa watoto ambao hushiriki katika mchakato wa kesi mahakamani hukumbwa na changamoto za tofauti za kimamlaka zinazoathiri jinsi wanavyowasiliana. Wanasema kuwa watoto hawa hushindwa kusimulia matukio kwa uhuru, hujibu maswali nje ya muktadha na hujikita katika kutoa majibu mafupi ya kukubali ambayo wakati mwingine huwa ya kupotosha. Njeri et al. (2018) wanaibua maoni kuwa wataalamu wa kisheria pamoja na walalamishi katika kesi ambao mara nyingi huwa hawajawakilishwa na mawakili hulazimika kutumia mikakati ya mawasiliano kama vile urudaji na uundaji upya wa maswali ili kuwawezesha kufikia maelewano katika mawasiliano. Kwa kuongezea, Richard na Nwizug (2017) wanasema kuwa wahusika wanaoshiriki mawasiliano mahakamani, kama mashahidi, mara nyingi hulazimika kujibu maswali kwa njia ambayo itawaridhisha mawakili. Pamoja na mchango wa tafiti hizi, kuna hitaji la kuchunguza jinsi wahusika hujenga mazingira ya kirafiki ya mawasiliano licha ya tofauti hizi za kimamlaka baina yao.

Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Ujihusishaji iliyoasisiwa na Giles (1973) na kuendelezwa na Giles et al. (1991). Nadharia hii inaeleza kuwa wahusika katika kikundi fulani cha mawasiliano hufanya mabadiliko katika matumizi yao ya lugha kulingana na muktadha wa mazungumzo. Nadharia hii ilitokana na nadharia ya mawasiliano katika usemi ambayo ilichunguza kile kinachosemwa na wanakikundi. Giles et al. (1991) wanaeleza kuwa nadharia hii sasa imepanuka na haishughulikii vipengele vya unenaji pekee. Wanasema kuwa vipengele vingine ambavyo si vya unenaji, kama vile viziada vya lugha na ishara za mwili, sasa vinazingatiwa katika kuchunguza ujihusishaji wakati wa mazungumzo baina ya wazungumzaji.

Giles et al. (1991) walijikita zaidi katika muktadha wa mawasiliano baina ya wasemaji. Wanasema kuwa muktadha wa mawasiliano ndio huchochea mabadiliko katika lugha itakayotumiwa pamoja na mtindo wa mazungumzo. Hii inaonyesha kuwa wazungumzaji hufanya mabadiliko ya kimaongezi kulingana na muktadha wa mazungumzo na malengo yao ya kuwasiliana. Nadharia hii iliufaa utafiti huu kwa sababu ilisaidia katika kuchunguza ujihusishaji unaojitokeza kupitia mikakati ya mawasiliano kwenye mahakama.

Nadharia hii pia imeainisha aina mbili za ujihusishaji: ujihusishaji wa makutano na ujihusishaji wa mwachano. Giles et al. (1991) wanabainisha ujihusishaji wa makutano kama njia ya kuonyesha utangamano wa kijamii. Makutano hurejelea namna wazungumzaji hubadilisha njia zao za kujieleza ili kudhahirisha ujihusishaji wao kupitia usemi, ishara au mabadiliko ya sauti. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, mtu anaweza kuamua kuacha tabia fulani kwa hiari yake ili kuimarisha mawasiliano kati yake na wengine anaowasiliana nao. Kwa upande mwingine, ujihusishaji wa mwachano ni mbinu ambapo wanakikundi hufanya mabadiliko ya kimaongezi ili kujitenga na washiriki wengine katika kikundi cha mawasiliano. Hapa, mnenaji anaweza kujitenga kutegemea nia yake katika mawasiliano. Ikumbukwe kuwa msemaji anaweza kuonyesha makutano katika kiwango kimoja na mwachano katika kiwango kingine. Hivyo, utafiti wa sasa ulichunguza namna mawakili, hakimu, walalamishi na mashahidi katika kesi za mizozo kwenye mahakama walivyojihusisha kupitia lugha iliyotumika.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kiuchambuzi wa kithamano. Utafiti ulifanywa katika Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu, kwani ndiyo mahakama maalumu inayosikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za migogoro ya ardhi. Kundi lengwa lilikuwa kesi sita zilizokuwa zimeratibiwa kusikizwa katika mahakama hiyo mwezi wa Oktoba 2019. Kipindi hiki kilichaguliwa kwa sababu kilikuwa na data ya hivi karibuni kufikia wakati wa utafiti. Sampuli ya utafiti ilijumuisha kesi nne za migogoro ya umiliki wa ardhi. Kesi hizi zilichaguliwa kwa kutumia usampulishaji wa dhamira kwa sababu ziliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili na zilitengewa muda mrefu wa mawasiliano ikilinganishwa na vikao vingine. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchunguzi usio wa kushiriki. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kushuhudia moja kwa moja na kurekodi mawasiliano kama yaliivyofanyika.

Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa yaliyomo (content analysis). Mawasiliano ya kesi yaliyorekodiwa yalinukuliwa, kisha kuchujwa kwa kutumia orodha ya uchambuzi ili kubainisha mikakati ya mawasiliano iliyotumika. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kimaandishi yaliyoambatana na nukuu halisi za washiriki, na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Ujihusishaji (Giles et al., 1991). Maadili ya utafiti yalizingatiwa kwa ukamilifu. Mtafiti alipata idhini kutoka kwa vitengo husika kabla ya kuanza utafiti. Mawasiliano ya kesi yaliyorekodiwa na kunakiliwa yalihifadhiwa kwa usalama ili kuzuia matumizi yasiyoidhinishwa. Ili kulinda siri na utambulisho wa washiriki pamoja na vipande vya ardhi vilivyohusika, mtafiti alitumia nambari na herufi za kialfabeti. Isitoshe, data iliyokusanywa ilitumika kwa madhumuni ya utafiti huu pekee.

MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulichunguza mawasiliano baina ya walalamishi, washtakiwa, mashahidi, karani wa korti, mawakili na hakimumu. Japo makundi haya ya watu yalitumia lugha ya Kiswahili, baadhi yao walitumia Kiswahili kisicho sanifu. Mazrui (1995) anaibua maoni kuwa Kiswahili ni lugha ambayo hubadilika kulingana na mazingira ya kimatumizi na hivyo matumizi yake hayawezi kufungwa ndani ya misingi ya usanifu pekee. Kwa misingi hii, utafiti huu umechunguza lugha hii namna ilivyotumiwa na washiriki hawa ili kudumisha uhalisia wa mazungumzo.

Ilibainika kupitia utafiti huu kuwa, mkakati wa usimulizi ulitumiwa na mashahidi, washtakiwa, mawakili pamoja na walalmishi ili kusimulia mfuatano wa matukio. Mawakili aghalabu waliwaongoza washiriki wengine katika masimulizi kwa kuwauliza maswali ya moja kwa moja. Kwa mfano:

Wakili: Unaweza kumbuka kesi ya Y ilikuwa namba gani?

Mlalamishi: Nilipeleka kesi ya criminal, mashtaka ya jinai Y.

Wakili: Na huko Y korti iliamua nini?

Mlalamishi: Kabla haijaamua iliniambia kuwa baada ya kutoa ushahidi wote nisirejee kortini tena. Korti itatafuta saveya kutoka kwa kaunti.

Wakili: Alifanya hivyo?

Mlalamishi: Akaniambia nitoe pesa. Nikatoa pesa akaniambia kama hutakubali ushahidi wa saveya mimi sitapata saveya mwingine. Nitoe pesa atafute saveya anayeamini. Nilitoa pesa, risiti ya pesa niliyotoa iko hapo. Ilikaa muda nikaambiwa nisubiri hadi wiki tatu nisirudi kortini, atakuja yeye na hao korti pamoja na huyo saveya. Baada ya kuona kuwa wiki ya nne inaingia nilikwenda huko Y nikakuta bwana huyo jaji alishahamishwa.

Wakili: Mwisho wake soroveya alitengeneza report?

Mlalamishi: Mwisho wake nikaambiwa kesi imeshakwisha bila mimi kujua. Ndipo nilipotafuta ilikwisha vipi.

Wakili: Ulipata iliishaje?

Mlalamishi: Eti mimi ndio nitafute saveya kutoka kaunti aje athibitish mpaka wa shamba langu lililokuwa limegeuzwa na kuwa dispute. Nilifanya hivyo kuenda kutafuta saveya wa kaunti akaja.

Wakili: Okey, huyo soroveya wa kaunti aliwahi kuandika ripoti?

Mlalamishi: Aliandika.

Wakili: Na hii ndiyo ripoti unasema aliandika akapeleka huko kortini Y?

Mlalamishi: Alipeleka kortini Y.

Wakili: Na baadaye sasa ulichukua hatua gani baada ya kupata hiyo ripoti ya soroveya na kesi imeisha Y?

Mlalamishi: Nilikuja kupata haki kwenye korti kuu. Yule mama aliendelea kutaka

*nisipite hata hiyo shamba langu,
anaendelea kupalilia.*

Usimulizi wa aina hii ulimpa mlalamishi nafasi ya kutosha ya kujieleza na kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu alivyowasilisha kesi kortini na maagizo aliyopewa na korti. Nafasi hii ilimwezesha mlalamishi kuwasilisha hoja zake kwa kina, kwa mpangilio na kwa uwazi bila kukatizwa; hali inayorahisisha uelewa wa matukio kwa wahusika wengine kwenye mahakama. Uhuru wa usimulizi katika mfano huu unabainika kupitia lugha ambapo mlalamishi anatumia nafsi ya kwanza katika usimulizi wake. Mlalamishi anatumia maneno kama vile *nikatoa, nilitoa, nilikwenda, nilifanya* na *nilikuja* katika usimulizi. Hapa, matumizi ya nafsi ya kwanza yametumika kuonyesha ushiriki wa kibinafsi wa mlalamishi katika usimulizi wake. Hii inafanya usimulizi uwe wa moja kwa moja na hivyo kuchangia katika kujenga mtiririko wa matukio yenye mshikamano ambayo anasimulia.

Isitoshe, kupitia kwa mkakati wa usimulizi mlalamishi ana uhuru wa kuongeza maelezo ya ziada. Kwa mfano:

Wakili: Na huko Y korti iliamua nini?

Mlalamishi: Kabla haijaamua iliniambia kuwa baada ya kutoa ushahidi wote nisirejee kortini tena. Korti itatafuta saveya kutoka kwa kaunti.

Hapa, mlalamishi hakubaki tu kwenye jibu aliloulizwa, bali aliongeza maelezo kwenye usimulizi wake kuhusu maagizo aliyopewa kabla ya maamuzi kutolewa na mahakama. Aidha, ametumia neno 'kabla' kama kiashiria cha mpangilio wa matukio ambapo analinganisha matukio ya kabla na baada ya maamuzi kutolewa. Isitoshe, kupitia mkakati wa usimulizi mlalamishi anatumia aya ndefu za usemi pamoja na kushirikisha maelezo kwa njia ya mfuatano. Aya ndefu ni ishara ya wakili kutomkatiza usemi mlalamishi huku maneno anayotumia mlalamishi kama vile *mwisho, na baadaye* yakaashiria mfuatano wa matukio ambayo yanaimarisha uhalisia wa ushahidi wake.

Vilevile, wawasilianaji walishirikisha urudiaji hasa wa vitenzi pamoja na baadhi ya istilahi katika mawasiliano hayo. Kwa mfano:

Hakimu: Hajasema ameenda wapi? Anasema mmeuza shamba ya marehemu.

Mshtakiwa: Your honour...

Hakimu: Kile anataka tu ni mumpatie makaratasi mlitumia kuuza hio shamba

na mumuonyeshe mliuza namna gani hilo shamba.

Mshtakiwa: Your honour jamaa alikuwa...

Hakimu: Sorry?

Mshtakiwa: Jamaa niliuzia hio shamba alikuwa na taabu sana ya mahali ya kukaa. Kaplot ndio nilimpa... Y kwa jina ya X. X ni cousin yangu. Iko parcels mbili inakamatana aliomba mimi ya kwamba please hii yangu ni kidogo ongeza mimi yako iwe pamoja. Sasa nikakata. Yangu nusu anakalia na yake akampa mimi. Mpaka wa leo bibi ya X aliniapproach yeye akasema yuko kwa land ya X. Hiyo naye iko kwa muhuri yangu. Shauri yangu mamake anakalia. Isitoshe huyu ni sister-in-law yangu bwana yake anaitwa X na huyu X naye ni ndugu yangu.

Hakimu: Hiyo shamba, hiyo Y ndiyo uliuzia?

Mshtakiwa: Hatukuza shamba yote your honour. Tuliuzia huyu jamaa nusu nusu ata iko demarcation kwa boma yake kuonyesha vile alikata. Hii mambo ya kusema tuliuzia yote hatujui kitu. Hata mawitnesses wote hawajui, ata kama tunaona mawitnesses hapa tulikataza. Hizo parcels zote demarcation iko ata watu wa area hii wanajua vizuri sana ata bibi ya mum anajua kuwa huyu jamaa ako na area yake ambao sijakataa kumpa yeye.

Hakimu: Mmelipa?

Mshtakiwa: Eeh, your honour.

Hapa, hakimu pamoja na mshtakiwa wanarudiarudia kitenzi 'kuuza shamba' naye mshtakiwa anarudiarudia istilahi 'your honour' mara kwa mara katika kauli zake anapomrejelea hakimu. Urudiaji huu unajitokeza katika hatua mbali mbali za usimulizi katika data hii. Kwamba, agahalabu hakimu alishiriki urudiaji alipotaka ufafanuzi kupitia maswali yake kwa mshtakiwa. Mshtakiwa kwa upande wake alishiriki urudiaji wa kitenzi 'kuuza shamba' alipokuwa akieleza muktadha wa tukio la kuuza shamba ambalo lilihusiana na kesi hii.

Aidha, mkakati wa maswali ulitumika katika mawasiliano ya kesi hizo kama ifuatavyo:

Wakili: Babako ako wapi kama ni babako?

Mlalamishi: Amekufa.

Wakili: Amekufa. Eleza mahakama shamba imesajiliwa kwa jina la nani. Kwa jina la baba ama kwa jina la...

Mlalamishi: ... (Kimya)

Wakili: Jibu!

Mlalamishi: Ushataja majina mengi mimi hapana jua.

Hakimu: Jibu swali uliloulizwa!

Wakili: Nimekuuliza shamba imesajiliwa kwa jina lako ama la baba yako?

Hakimu: Shamba liko kwa jina la nani?

Mlalamishi: Director. Sijui jina vizuri. Alisema jina kama korti inaendelea.

Hakimu: Jibu swali kama unaelewa. Kama huelewi unasema. Shamba imesajiliwa kwa jina la nani?

Wakili: Jina ya?

Mlalamishi: Ya hiyo company.

Wakili: Kama unasema shamba imesajiliwa kwa jina ya director wa hio kampuni, niaje tena imekuwa shamba ya babako?

Mlalamishi: Awali ukiendelea kuniuliza majina kama hiyo...

Wakili: Nimesema, umeelezea mahakama hapo awali kuwa shamba imesajiliwa kwa jina la baba yako tena umesema imesajiliwa kwa hiyo kampuni. Sasa nichukue gani? Nichukulie kuwa shamba iko chini ya jina la baba?

Mlalamishi: Wewe ulianza kuniuliza majina kama hata sijui. Nimekwambia ata sheria ya land hakuna.

Matumizi ya mkakati wa maswali yanajitokeza kupitia mawasiliano kwenye data hii. Wakili anauliza mlalamishi maswali kadha wa kadha kwa mfululizo. Kwa mfano anauliza:

Babako ako wapi kama ni babako? Shamba limesajiliwa kwa jina la nani? Sasa nichukue gani?

Maswali haya yanajitokeza katika hatua mbali mbali za mahojiano baina ya wakili na mlalamishi. Hakimu pia, anaendeleza mawasiliano kwa kushirikisha maswali anayoyaelekeza kwa mlalamishi. Anauliza: *Shamba liko kwa jina la nani? Swali hili aidha limeulizwa tena na kurejelewa kwa miundo mingine tofauti kwa mfano: 'Jina ya?' na 'Shamba limesajiliwa kwa jina la nani?'*. Kwa kurejelea data hii, maswali aliyouliza wakili yalifuatanishwa pasi na kutolewa kwa majibu ya moja kwa moja. Maswali hayo yalifanana japo yaliulizwa kwa

namna tofauti katika mahojiano hayo. Shahidi kwa upande wake anakimya na kutotoa majibu yanayolingana na maswali anayoulizwa. Vilevile, wakati mwingine majibu yake yalijitokeza kwa kauli fupi kama *'Amekufa'* na *'Sijui jina vizuri'*. Hata hivyo majibu mengineyo yalijitokeza kama kauli ndefu katika baadhi ya vipindi. Kimsingi, mkakati wa maswali ulijitokeza kupitia maswali ya moja kwa moja'.

Mkakati mwingine ni ukatizaji wa usemi. Pratt (1977) anabainisha kuwa ukatizaji wa usemi ni jambo la kawaida na muhimu katika mazungumzo yoyote. Pratt anaieleza kuwa ni vigumu kufuata kanuni ya kusubiri mtu mmoja amalize usemi wake ndipo mwingine aanze kuzungumza. Licha ya urasmi na sheria zinazoongoza mazungumzo katika mahakama, mkakati wa ukatizaji wa usemi ulidhihirika katika mawasiliano hayo kama ifuatavyo:

Wakili: Mzee.

Mlalamishi: Enhe.

Wakili: Unajua kiasi ya shamba namba Y?

Mlalamishi: Ilipimwa.

Wakili: Wewe unajua? Sasa imekuwa moto!

Mlalamishi: Ikuwe moto?

Wakili: No, you are now...

Mlalamishi: Mimi sikupima shamba langu.

Wewe unataka ikuwe moto...

Wakili: Unajua parcel namba...

Mlalamishi: Ngonjea...

Hakimu: Umeulizwa unajua size ya...

Mlalamishi: Card inaonyesha eneo la shamba la Y mwenyewe anayo. Mimi siwezi kujua.

Mimi najua...

Hakimu: Ile hujui sema hujui. Umeulizwa...

Mlalamishi: Sijui.

Hakimu: Ndio anakuuliza hujui size?

Mlalamishi: Size yake sijui.

Hapa, mkakati wa ukatizaji usemi ulijitokeza katika mawasiliano baina ya wakili, hakimu na mlalamishi. Wakili alimkata usemi mlalamishi kwa kuingilia kati na kumuuliza maswali mengine. Kwa mfano:

Mlalamishi: Mimi sikupima shamba langu. Wewe unataka ikuwe moto...

Wakili: Unajua parcel namba...

Inabainika katika mfano huu kuwa swali la wakili linaulizwa pasi na mlalamishi kukamilisha kuwasilisha kauli yake. Pia swali hili limechukua mwelekeo tofauti

na kauli anayoendelea kutoa mlalamishi. Hakimu pia ana uhuru wa kushiriki ukatizaji usemi anapoingilia mazungumzo yale na kuuliza mlalamishi swali: *Umeulizwa unajua size ya...* na *'Ile hujui sema hujui. Umeulizwa...'* Kwa mujibu wa data hii, mlalamishi aliingilia mazungumzo kwa kutoa kauli yake anaposema: *'Tkuwe moto?'* na *'Mimi sikuuza shamba langu...'* Ukatizaji usemi unaobainika katika data hii ulijitokeza katika vipindi vingi vilivyohusisha maswali na majibu na uliambatana na maswali ya moja kwa moja. Mkakati wa ukatizaji usemi ulijitokeza katika tukio lingine kama ifuatavyo:

Wakili: Wewe umewahi kuchukua mahakama akuwekee kesi eti yeye anataka shamba? Mlalamishi:

Order imetoka hapa nendeni mkapime shamba hiyo. Sasa baada ya kupima shamba langu...

Wakili: Ama niulize hivi, wewe na X nani alichukua mwingine kortini? Najua unataka...

Hakimu: Mzee jibu swali vile umeulizwa. Amekuuliza swali. X ameshawahi kupeleka kortini kwa sababu ya hii shamba?

Mlalamishi: Bado.

Katika tukio hili, hakimu aliingilia maelezo ya wakili kabla ya kauli yake kukamilika na kurudia swali kwa mtindo wa kushirikiza ili jawabu kuhusu ni nani kati ya wahusika alikuwa amefikisha malalamishi mahakamani. Hapa, hakimu anasisitiza umuhimu wa kutoa jibu badala ya kuendelea na maelezo mengi ambayo hayaendani na maswali yaliyoulizwa. Katika mahojinao haya, ukatizaji usemi unajitokeza kama mkakati wa mawasiliano uliotumika na washiriki katika mawasiliano kwenye mahakama.

Kwa upande mwingine, mkakati wa mahojiano ulitumika katika kesi za umiliki wa ardhi kwenye Mahakama ya Mazingira na Ardhi ya jijini Kisumu kama ifuatavyo:

Wakili: Ni page ngapi? Hiyo judgement ni pages ngapi? Hiyo judgement?

Mlalamishi: Hukusoma wewe?

Wakili: How many pages of the judgement?

Hakimu: Ilikuwa pages ngapi? Unajua mambo mengine ujibu vile umeulizwa.

Wakili: Ni pages ngapi? Hii tu? Hebu angalia document. Ngapi? X, nimekuonyesha

pages ambazo utaangalia. Hizo ni makaratasi yangu ya file.

Mlalamishi: Sasa hii page unataka ya nini?

Wakili: Nataka uhesabu hiyo page ambayo imeandikwa judgement. Ni page ngapi?

Mlalamishi: Page moja u nusu. Moja unusu.

Wakili: Moja u nusu.

Data hii inaonyesha kuwa kupitia mkakati wa mahojiano mahakamani, mawakili walitumia maswali ya moja kwa moja ili kupata taarifa maalum kutoka kwa walalamishi. Wakili na hakimu wanauliza urefu wa hukumu iliyokuwa imetolewa kwa kutumia maswali ya kurudiarudia ambayo pia ni ya moja kwa moja. Kwa mfano: *"Ni page ngapi? Hiyo judgement ni pages ngapi? Ilikuwa pages ngapi?"*

Hali hii inaonyesha namna maswali yaliundwa upya mara kadha na wakili pamoja na hakimu ili kuweza kupata jibu sahihi. Isitoshe, mlalamishi anatoa majibu yake kwa njia ya kuhoji badala ya kutoa majibu ya moja kwa moja. Kwamba, mlalamishi anageuza mwelekeo wa mahojiano na kumuuliza wakili swali badala ya kujibu maswali anayoulizwa moja kwa moja. Mathalan anahoji: *"Sasa hii page unataka ya nini?"* Hili ni kinyume na anavyotarajiwa katika kuwasilisha hoja zake mahakamani na si mara nyingi ambapo hali hii hutokea katika mawasiliano mahakamani. Hali hii inachochea wakili kuzidi kurudia swali lake upya na kulirudia tena na tena. Pia, mahojiano katika data hii yanaonyesha matumizi ya mbinu ya kuchanganya lugha ambapo lugha ya Kiswahili pamoja na Kiingereza inatumika katika kuendeleza mkakati wa mahojiano. Kitendo hiki kinafanywa na wahusika wote ambao ni wakili, mlalamishi na hakimu na kinamchochea mlalamishi kutoa majibu mafupi kama *'moja na nusu'* ambayo yanatokana na kutumika kwa mfululizo wa maswali.

Mkakati wa maombi ya kisheria ulitumika katika mawasiliano kama ilivyo katika mfano ufuatao:

Wakili: Na sasa vile umekuja, unaomba korti ikusaidiaje?

Mshtakiwa: Naomba korti inipatie mimi shamba maana hiyo shamba nimeshalima kwa miaka mingi na sasa bado nailima. Mimi ndiye nailima

Data hii inaonyesha kwamba mawakili walitumia maswali ya maombi ya wazi ili kumwelekeza mshtakiwa kutoa ombi lake moja kwa moja mbele ya mahakama la kutaka korti imfanye mmiliki halali wa shamba hilo.

Hapa, muundo wa kauli za moja kwa moja unatumika haswa mshatakiwa anaposema, *'Naomba korti inipatie mimi shamba'*. Kwa mujibu wa swali la wakili, mshtakiwa alihitajika kutoa ombi lake kwa uwazi pamoja na sababu za kudai haki hiyo. Isitoshe, matumizi ya mkakati huu yanafungua nafasi ya mshtakiwa kujieleza kwa uhuru na kwa uwazi. Aidha, inabainika katika data hii kwamba mkakati wa maombi unatokea wakati wa ushahidi ambao huwa sehemu ya mwisho ya mawasiliano ya kesi mahakamani.

Majadiliano

Matokeo haya yanaonyesha kuwa mkakati wa usimulizi katika mawasiliano kwenye mahakama hayatekelezi jukumu la kutoa taarifa pekee, bali pia kama mchakato wa kimkakati unaoathiriwa na tofauti za kimamlaka baina ya washiriki. Ilibainika kuwa mkakati huu ulitumika hususan na walalamishi katika kusimulia mfuatano wa matukio ya mizozo. Nadharia ya Ujihusishaji (Giles et al., 1991) hudai kuwa wazungumzaji hufanya mabadiliko ya kimaongezi ili wafanane ama wajitenge na washiriki wengine katika kikundi wanachoshiriki mawasiliano. Kwamba, washiriki ambao walikuwa wenye mamlaka ya chini katika kikundi hicho cha mawasiliano, walibadilisha na kupanga maongezi yao ili yaendane na matarajio ya mahakama hiyo kupitia usimulizi. Mabadiliko haya yalijitokeza katika namna walalamishi walivyowasilisha simulizi zao kwa uzito zaidi kuliko ujumbe waliokuwa wanawasilisha. Hali hii ilibainika kupitia walivyoongeza maelezo ya ziada katika usimulizi wao, matumizi ya nafsi ya kwanza na pia kutumia aya ndefu za usemi katika uwasilishaji. Rock (2020) anasema kuwa simulizi katika miktadha ya kisheria huudwa chini ya shinikizo la kitaasisi ambapo ufanisi wa ushahidi hutegemea zaidi jinsi ujumbe unavyowasilishwa kuliko ujumbe. Hivyo mabadiliko ya kimaongezi yaliyobainishwa yanaweza kutafsiriwa kama kama juhudi za kuoanisha masimulizi yao na mfumo wa mahakama. Matokeo yameonyesha kuwa, kupitia kwa mkakati wa usimulizi, suala la mamlaka haliweza kupimwa kwa kuzingatia anayezungumza bali kwa kuangazia namna mazungumzo yanavyopangwa na kuwasilishwa.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa mkakati wa maswali ulitumika kwa kiasi kikubwa katika mawasiliano haswa na mawakili na hakimumu. Hale (2010) anasema kuwa maswali katika muktadha wa mahakama husaidia katika kuhakikisha kwamba mawasiliano ni sahihi. Hata hivyo, mkakati huu haukutumika tu kusahilisha mawasiliano wala kupata taarifa bali

mawakili na hakimumu waliutumia kama nyenzo ya kushurutisha na kuchuja taarifa ya mashahidi ama walalamishi. Matokeo yamebainisha kuwa mkakati wa maswali uliathiri majibu yaliyotolewa na walalamishi na kuvuruga mtiririko wa hoja zao huku wakilazimika kuzielekeza upya na kuwafany awakati mwingine wanyamaze. Hali hii iliashiria ujihusishaji wa mwachano ambapo wahusika hujihusisha kwa kujitenga na kuonyesha ukosefu wa upatanishaji wa mazungumzo. Matokeo haya yanaonyesha kuwa wahusika wanapokosa kupatana kimawasiliano si ishara ya hitilafu katikamawasiliano. Yaweza ikawa ni mkakati wa mawasiliano unaotumika na wahusika kulinda taswira zao pamoja na kujenga hatua ya kufikia makubalianao y amaana katika mawasiliano.

Ingawa mkakati wa ukatizaji usemi mara nyinigine hutumika kwa ushirikiano, katika baadhi ya matukio katika utafiti huu ulibainika kutumika kuashiria ujihusishaji wa mwachano. Hii ni hali ambapo mzungumzaji hujiondoa au hujitenga katika kikundi anachoshiriki mazungumzo (Giles et al., 1991). Hili lilibainika kulipokosekana ulinganifu wa kimazungumzo na ushindani wa kimawasiliano baina ya wahusika. Hapa, mawakili waliwakata kauli walalamishi ili kusisitiza kutolewa kwa majibu badala ya maelezo mengi huku wakitumia lugha ya ushurutishaji walipouliza maswali. Kwa upande mwingine, walalamishi walionyesha ujihusishaji wa mwachano walipovunja mtiririko wa mazungumzo na kuwakata mawakili kauli ili kupinga dhana za wakili na kutaka kuanzisha usimulizi wake binafsi. Hii ina maana kwamba, mkakati huu unapotumika katika mahakama haupaswi kuonekana kama mbinu ya kimaongezi bali kama kiashiria cha mahusiano ya kimamlaka ndani ya mawasiliano. Kwamba, tofauti za kimamlaka baina ya wazungumzaji zinadhihirikakupitia kujitenga huku.

Mkakati wa mahojiano ulitumika kama chombo cha kudhibiti mwelekeo wa mawasiliano katika mahakama hii. Hili lilibainika ambapo wakili na hakimumu walichukua nafasi kuu katika kuongoza mwelekeo wa majibu ya wahusika wengine kama walalamishi na mashahidi. Matumizi ya mbinu ya kuchanganya lugha ambapo wakili na walalamishi walichopeka maneno ya lugha ya Kiingereza walipowasiliana kwa lugha ya Kiswahili yanaweza kutafsiriwa kama ujihusishaji wa makutano. Washiriki hawa walipochanganya lugha hizi, walilenga kuimarisha maelewano baina yao. Hata hivyo walalamishi walipotoa majibu yao kwa njia ya kuhoji au kukwepa swali moja kwa moja, hali hii inaonyesha

ujihusishaji wa mwachano ikiashiria hali ya mlalamishi kujitenga au pia kupinga uhibiti wa wakili katika mawasiliano hayo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyeshakwamba mkakati wa mahojiano haukutumika tu kama njia ya kupata taarifa ama ushahidi, bali ulitumika kama chombo cha kudhibiti namna ya kujibu ambapo wahusika walielekezwa kutoa majibu mafupi yaliyolingana na mwelekeo wa wakili.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba mkakati wa maombi ya kisheria ulitumika na washiriki kama vile mashahidi kwa kuongozwa na mawakili katika kutoa maombi yao mahakamani. Utafiti huu ulibainisha kwamba uelekezi huu ulifanyika kupitia mbinu mahususi za lugha ambazo zilichangia katika kuundwa na pia kuchujwa kwa baadhi ya ushahidi mahakamani. Hali ya ujihusishaji wa makutano ilidhihirika pale mashahidi walipotumia lugha rasmi tena ya upole na unyenyekevu walipowasilisha maombi huku wakizingatia msamiati kama vile *'naomba korti'* ili kuimarisha hoja zao. Hii ina maana kwamba wakili na shahidi walijihusisha na kushirikiana kwa kujipanga kimkakati ili kuendana na matakwa ya makahama ya kushawishi na kueleweka. Kwa njia hii, ujihusishaji wa makutano ulichangia kuimarisha uhalali wa maombi ya shahidi ndani ya mfumo wa kisheria badala ya kuwa mawasiliano ya kawaida ya kijamii.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala hii imewasilisha matokeo na mjadala kuhusu mikakati ya mawasiliano katika kesi za mizozo

ya umiliki wa ardhi kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu. Mikakati mbalimbali imebainika kupitia kazi hii. Mathalani, usimulizi, maswali, ukatizaji usemi, mahojiano na maombi ya kisheria. Ilimebainika kupitia utafiti huu kwamba ujihusishaji wa makutano ulidhihirika kupitia mikakati ya mawasiliano ambayo iliawezesha wahusika kuimarisha maelewano, kupata ufafanuzi na kupunguza utata wa taarifa iliyotolewa. Mikakati hiyo ilikuwa usimulizi, mahojiano maombi y akisheria. Isitoshe, mikakati ambayo ilifichua mivutano katika tafsiri na uhusiano wa kimamlaka iliashiria kuwepo kwa ujihusishaji wa mwachano. Kupitia kwa lugha mikakati hii ilibainika kupitia majibu yaliyolingana na maswali, ukimya katika mazungumzo na maswali kuulizwa kwa mtindo wa ushurutishaji na shinikizo. Aghalabu mikakati hii ilikuwa maswali na ukatizaji usemi. Hivobasi, utafiti unahitimisha kuwa mawasiliano makahamani si ya moja kwa moja bali ni mchakato ambapo maana hujengeka kupitia mwingiliano wa kimuktadha kati ya ujihusishaji wa makutano na mwachano; ambapo maana hurekebishwa kutegemea mikakati ya mawasiliano inayotumika.

Mapendekezo: Makala haya yanapendekeza kuwa, mahakama ihimise wahusika katika kesi kupunguza kujihusisha kwa kujitenga ili kuimarisha mazingira ya kirafiki ya mawasiliano ambayo hukuza maelewano kupitia kwa mikakati inayochochea ujihusishaji wa makutano.

Marejeleo

- Anyonje, L. (2004). *Communication strategies in conflict resolution and management: A case study of urban slum dwellers with specific reference to Kibera slum of Nairobi, Kenya* (Master's thesis, University of Nairobi). <http://hdl.handle.net/11295/95816>
- Gibbons, J. (2003). *Forensic linguistics: An introduction to language in the justice system*. Blackwell Publishing.
- Giles, H., Coupland, J., & Coupland, N. (1991). Accommodation theory: Communication, context and consequence. In H. Giles, J. Coupland, & N. Coupland (Eds.), *Contexts of accommodation: Developments in applied sociolinguistics*. Cambridge University Press.
- Hale, S. (2010). *The discourse of court interpreting: Discourse practices of the law, the witness and the interpreter*. John Benjamins Publishing Company.
- Kiguru, G. (2014). *A critical discourse analysis of language used in selected courts of law in Kenya*. <http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/14017>
- Luchjenbroers, J. (1993). *Pragmatic inference in language processing* (Unpublished doctoral dissertation). La Trobe University.
- Magiri, M. C. (2019). *An analysis of alternative dispute resolution as a communication strategy in conflict resolution: A case study of court annexed mediation, Milimani Law Courts–Family Division* (Unpublished master's thesis). University of Nairobi.

- Matu, P. M., Odhiambo, K., Adams, Y., & Ongarora, D. (2012). *The court interpreters' role perception: The case of English–Dholuo interpreters in subordinate courts in Nyanza Province, Kenya*. *Greener Journal of Social Sciences*, 2(4), 121–126. <https://doi.org/10.15580/GJSS.2012.4.08091239>
- Mazrui, A. A., & Mazrui, A. M. (1995). *Swahili state and society: The political economy of an African language*. East African Educational Publishers.
- Njeri, K. N., Kiliku, P., & Kiai, A. (2018). Controlling courtroom discourse through linguistic manipulation: A case study of criminal trials at the Kibera Law Courts, Nairobi. *International Journal of Social and Development Concerns*, 2, Article 5/12. <http://www.ijfdc.org>
- Obange, N., & Wagah, G. G. (2019). Land tenure challenges in Kisumu City, Kenya. *Net Journal of Social Sciences*, 7(4), 85–91. <https://doi.org/10.30918/NJSS.74.19.023>
- Odera, J., Achieng, L., & Ochieng, R. O. (2019). Linguistic strategies employed during examination of children in conflict with the law in Eldoret Children's Court, Kenya. *Journal of African Interdisciplinary Studies*. <https://s11nk.com/fjvzzbm>
- Opeibi, T. (2012). Language countertrading in courtroom exchanges in Nigeria: A discursive study. *International Journal of Applied Linguistics and English Literature*, 1(5), 49–63. <https://doi.org/10.7575/ijalel.v1n.5p.49>
- Pratt, D. D. (1997). *Five perspectives on teaching in adult and higher education*. Krieger Publishing Company.
- Richard, B., & Nwizug, S. S. (2017). A Critical Discourse Analysis of Courtroom Proceedings in Nigeria. *AFRREV IJAH: An International Journal of Arts and Humanities*, 6(4), 93–102. <https://doi.org/10.4314/ijah.v6i4.8>
- Rock, F. (2020). Forensic linguistics. In J. Culpeper, M. Haugh, & D. Kádár (Eds.), *The Palgrave handbook of linguistic (im)politeness* (pp. 623–642). Palgrave Macmillan.
- Seedhouse, P. (2004). *Conversation analysis of institutional talk: Methods and practices*. Palgrave Macmillan.
- Selinker, L. (1972). Interlanguage. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, 10(1–4), 209–231. <https://doi.org/10.1515/iral.1972.10.1-4.209>
- Widodo, A. (2025). Courtroom communication: Identification of the communication characteristics of criminal trials in Indonesian courts. *Frontiers in Communication*, 10, Article 1623307. <https://doi.org/10.3389/fcomm.2025.1623307>